**HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI MHE. JAJI DKT. ELIEZER MBUKI FELESHI KATIKA MWENDELEZO WA MAFUNZO KWA BAADHI YA WATUMISHI WA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI NA KIKAO KAZI CHA FARAGHA CHA VIONGOZI WA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA SHULE YA UONGOZI YA MWL. NYERERE KIBAHA MKOANI PWANI KUANZIA TAREHE 16 HADI TAREHE 20 JANUARI, 2024**

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

**Dkt. Boniphace Nalija Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bw. Mark Eldad Mulwambo, Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Wakurugenzi na Wakuu wa Idara na Vitengo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Wakurugenzi Wasaidizi na Mawakili Wafawidhi Ofisi za Mikoa;**

**Wawakilishi wa Mawakili wa Serikali na Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Wawezeshaji na Watoa Mada;**

**Wageni Waalikwa;**

**Waandishi wa Habari;**

**Mabibi na Mabwana.**

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

## 1. UTANGULIZI

**Ndugu Viongozi na Washiriki wa Mafunzo;**

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutukutanisha katika ukumbi huu kwa ajili ya kuanza mafunzo yatakayoambatana na Kikao Kazi cha Faragha.

Kwa namna ya pekee nipende pia kushukuru uongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kunipa fursa hii ya kutoa hotuba hii leo tarehe 17 Januari, 2024 katika mwendelezo wa mafunzo ya pamoja na kikao kazi vilivyopangwa kufanyika tarehe 16 – 20 Januari, 2024. Nilitamani kuwepo wakati wa ufunguzi wa mafunzo haya jana tarehe 16 Januari, 2024 lakini nilishindwa kutokana na sababu zilizokuwa nje ya uwezo wangu.

**Ndugu Viongozi na Washiriki wa Mafunzo;**

Mafunzo haya ni muhimu sana katika kudumisha ufanisi uliopo katika Taasisi zetu, lakini pia yanakusudia kuwanoa Viongozi wa kisheria na wa kada nyingine katika taaluma ambayo inakua kila siku na hivyo kuhitaji mafunzo mapya ili kuendana na mabadiliko katika taaluma ya sheria na sekta nyingine nchini na duniani kote.

Ni katika umuhimu huo, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeona umuhimu wa kuwa na wakufunzi ambao ni Majaji ambao bado wapo kazini (Sitting Judges) pamoja na wakufunzi wabobezi kwenye maeneo mbalimbali ili kutoa mafunzo haya muhimu kwa Viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Kwa namna ya pekee

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

napenda kuwapongeza viongozi wa Taasisi zote zilizohakikisha Mawakili wao wa Serikali wanashiriki katika mafunzo haya muhimu. Nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa kuteuliwa na Taasisi zenu kushiriki na kuhakikisha mmefika hapa bila kukosa. Hongereni sana.

## 2. LENGO LA MAFUNZO

**Ndugu Viongozi na Washiriki wa Mafunzo;**

Katika barua ya mwaliko na katika utangulizi wa shughuli hii, nimefahamishwa kuwa lengo kuu la mafunzo haya ni kuwapatia baadhi ya Mawakili wa Serikali waliopo hapa pamoja na menejimenti ujuzi endelevu ili kuwaongezea ufanisi katika utendaji kazi wao pamoja na kuboresha mahusiano yao kama viongozi ambao ni nguzo kuu katika usimamizi wa shughuli za Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

HOTUBA YA MNANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Aidha, mafunzo haya yatasaidia kuwajengea uwezo hususan katika Uandaaji wa Kanuni na Miongozo kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi, kujifunza kwa ujumla kuhusiana na Mashauri ya Haki za Binadamu, masuala ya uhitimishwaji wa tuzo za Usuluhishi, kujifunza namna taasisi nyingine zinavyosajili na kusimamia Mashauri kupitia mifumo ya TEHAMA hususan Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pamoja na Mahakama ya Tanzania. Vilevile, mafunzo

haya yatawawezesha kupata ufahamu wa namna bora ya Uibuaji wa Miradi ya Maendeleo na Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti sambamba na kutambua mambo muhimu ya Udhibiti Ubora.

**Ndugu Viongozi na Washiriki wa Mafunzo;**

Mafunzo haya pia yanajumuisha elimu ya uwekezaji hususan namna ya kuongeza kipato ikiwemo Ununuzi na Uuzaji wa Hisa, Uwekezaji katika Amana za Serikali, Vipande vya UTT, Hati Fungani pamoja na Uwekezaji katika Ardhi. Mafunzo haya yataongeza mwanga katika kupanua kipato kwa kila mmoja wetu na watumishi tunaowasimamia katika Ofisi zetu ambao kwa namna moja au nyingine, taaluma hii ya uwekezaji bado ni ngeni kwao. Mtumishi wa umma anapokuwa na vyanzo vya mapato nje ya mshahara itamsaidia kuongeza ufanisi katika kujihudumia pamoja na wale wanaomtegemea bila kuathiri ubora wa kazi yake ya ajira.

**Ndugu Viongozi na Washiriki wa Mafunzo;**

Natumaini na kutarajia kuwa washiriki wote mtayafuatilia na kushiriki ipasavyo mafunzo haya ambayo ni ya muhimu sana kwenu pamoja na watumishi ambao hawakuweza kujumuika ili kupata mafunzo haya. Nawaasa kuyachukulia kwa uzito na umuhimu wake ili kufanya lengo la mafunzo kutimia kwa asilimia zote na kujiweka vizuri katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

## 3. LENGO LA KIKAO KAZI CHA FARAGHA

**4. Ndugu Viongozi na Washiriki wa Mafunzo;**

Nimejulishwa kuwa baada ya mafunzo haya kutakuwa na kikao kazi cha Faragha ambacho kitafanyika kwa siku mbili. Lengo kuu la vikao vya namna hii ambavyo hufanyika mara chache sana katika mwaka ni kufanya tathmini ya namna shughuli za taasisi zilivyoendeshwa. Niwapongeze menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuweza kufanya hivi kwa miaka takribani mitatu mfululizo.

**Ndugu Viongozi na Washiriki wa Mafunzo;**

Nichukue fursa hii kuwasisitizia kuhusu kuweka umuhimu na kushiriki ipasavyo kwa kutoa michango mbalimbali katika Kikao kazi ambacho mnatarajia kufanya. Katika kikao hicho mtapata fursa ya kupitia Mpango na bajeti ya Ofisi yenu pamoja na utekelezaji wa mpango huo. Shughuli zetu hutegemeana na bajeti ambayo kimsingi inapangwa kupitia fursa kama hizi ambapo hufanyika tathmini ya utendaji kazi na kuangalia mambo muhimu yanayohitaji nyongeza ya bajeti na kadhalika; tumieni wasaa huu kushauri vizuri na kutoa mapendekezo ambayo yataongeza ufanisi katika shughuli za kila siku ili ubora wa ofisi uendelee kuonekana.

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Pia, nimeelezwa kuwa kutakuwa na mtaalamu wa saikolojia pamoja na wabobezi katika masuala ya maadili. Naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa namna mlivyopanga mada hizi kwani hatuweza kuwa na watumishi wa umma wasio na maadili au wenye maadili hafifu katika utendaji wao wa kazi. Hili ni takwa la kisheria lakini pia ni takwa la kijamii ambapo lazima binadamu yeyote kuwa na maadili hususan katika utoaji wa huduma kwa jamii.

Nawakumbusha mawakili wa serikali wote kutilia maanani maadili yetu na kuchukua hatua bila kusita kwa wale wote watakaokwenda kinyume. Katika hili, Kanuni zetu za Maadili dhidi ya mawakili wanaokiuka maadili katika utekelezaji wa majukumu yetu-'The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Provision of Legal Opinion by State Attorneys and Law Officers in Public Service) Guidelines, G.N 32/2023.

Katika zama za leo, elimu kuhusu uongozi, akili, hisia na saikolojia ni masuala ya muhimu sana katika kuleta ufanisi kwa mtumishi wa umma hususan kiongozi. Sikilizeni kwa umakini mada hizo na kuuliza maswali wawasilishaji ambao ni wabobezi ili mtoke hapa mkiwa na afya njema ya akili na mbinu za uongozi zilizoboreshwa.

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

**Ndugu Viongozi na Washiriki wa Mafunzo;**

Kwa kutambua mahitaji ya nchi yetu nyakati hizi na fursa mliyo nayo katika mkutano huu sina budi kuwakumbusha kwa uchache mambo ya msingi, japo yanaweza kuonekana ya kawaida sana kwa wakili asiyejua maana, ambayo kila wakili wa Serikali huelekezwa kufungamana nayo katika utumishi wake. Mambo hayo ni : (1) kujifunza maarifa na stadi mpya za kazi bila kukoma, (2) kuandaa dondoo za mawasilisho ya kazi (submissions) na kuandika mrejesho wa mambo yaliyojiri katika kazi aliyofanya, (3) kuwahi eneo la tukio la kazi walau nusu saa kabla ya kuanza, (4) kuwa na mawasiliano na mahusiano yenye tija na wadau muhimu, (5) kutokutenda jambo/kutofanya uamuzi kwa jambo lililo nje ya maelekezo yaliyotolewa, (6) kuwa mwangalifu muda wote wakati wa kufanya mawasiliano iwe kwa maneno au maandishi, (7) kujilinda na kujitenga na uovu na kuwa mwadilifu muda wote, (8) kuwa tayari kutekeleza kazi/jukumu la ziada wakati wote na kutoacha ombwe la uwakilishi pale uwakilishi wa Serikali unapohitajika katika kipindi ambacho hakuna afisa mwingine amehudhuria, (9) kutekeleza majukumu yako huku ukiwasimamia na kuwajengea uwezo wa kazi maafisa walio chini yako na (10) kufanya utafiti siku zote. Ni matumaini yangu kwamba dondoo hizo

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

chache na nyingine mnaweza kuzirejea wakati wa tathmini mtakayofanya wakati wa Kikao cha faragha.

**Ndugu Viongozi na Washiriki wa Mafunzo;**

Napenda kuwafahamisha kwamba, kuelekea mwaka wa fedha 2024/25 tutaendelea na jitihada tulizoansisha mwaka 2022/23 na 2023/24 za kutumia mifumo ya Office of the Attorney General Management of Information System (Oagmis) na Public Employees' Management of Information System (PEPMIS) kupima utendaji kazi wa kila wakili wa Serikali. Kazi hii katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inashughulikiwa na Dawati lenye dhamana ya usajili wa mawakili, tathmini ya utendaji kazi za mawakili wa Serikali pamoja na mifumo wezeshi. Kurugenzi husika na Dawati hili watashirikiana ipasavyo na mamlaka ajiri kutekeleza jukumu hili.

Ninapenda kuwafahamisha kwamba, kufikia tarehe 16.01.2024, Daftari la Usajili wa Mawakili wa Serikali lilikuwa linaonesha kuwa sasa tunao jumla ya mawakili wa Serikali 3,365 (ikijumuisha mawakili 111 waliopo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, 128 waliopo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, 307 waliopo TAMISEMI na 661 waliopo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka).

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Aidha, ili kufikia lengo la kumjengea uwezo kila wakili wa Serikali na kumpatia stadi stahiki katika maeneo mbalimbali ya kazi, taratibu zitaandaliwa ili kila wakili apate fursa ya kutekeleza majukumu mengi ya kisheria ikiwemo stadi za kuendesha mashauri kwenye vyombo vya maamuzi. Lengo hili ninavyofahamu litafikiwa bila kuibua vikwazo vya kumwezesha wakili wa Serikali kujenga na kuhifadhi umahiri wake katika eneo la chaguo lake. Hatua hii inalenga kuwawezesha mawakili kukua, kubobea na kufikia ndoto zake za katika Utumishi wa Umma na maeneo mtambuka ndani na nje ya nchi (kwenye Taasisi za Kimataifa).

**Ndugu Viongozi na Washiriki wa Mafunzo;**

Baada ya kuwashirikisha haya niliyosema sasa naomba kutumia muda huu kuwaomba mzingatie malengo ya Mkutano huu kupitia Programu iliyoandaliwa. Aidha, nitafurahi kupata mrejesho wa mambo yatakayojiri katika Mkutano huu na naamini mtawashirikisha wenzenu pia mtakaporejea kwenye Ofisi zenu.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KAZI IENDELEE**

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.**

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI